**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

## KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI

**03 JULAI, 2015**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

### KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI – TAREHE 03 JULAI, 2015

## I. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

### 302. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANG'HWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Yuko Mkandarasi aliyeanza ujenzi wa barabara ya kutoka Busisi – Kharumwa – Nyang'holongo tangu mwaka 2011 lakini ametengeneza sehemu fupi tu ya mradi huo kupitia vijiji vya Nyamasale, Isole, Ngoma, Busolwa hadi kijiji cha Nyarugugumo:-

(a) Je, ni vigezo gani vilivyotumika kuajiri Mkandarasi asiye na uwezo;

(b) Je, Serikali imemchukulia Mkandarasi huyo hatua gani kwani sasa ni miezi 6 hayupo kwenye eneo la kazi yake;

(c) Tarehe 26/10/2010 Mhe. Rais alitoa pia ahadi ya ujenzi wa barabara hiyo ya Busisi – Nyangholongo; Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

**WIZARA YA MAMBO YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**303. MHESHIMIWA HAROUB MOHAMED SHAMIS (CHONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Hivi karibuni Rais wa Marekani aliutangazia ulimwengu juu ya kuuawa kwa Kiongozi wa Al-Qaida Osama bin Laden huko Pakistani katika mapambano ya kumkamata:-

Je, hali ya ugaidi ikoje hapa nchini na Duniani kwa ujumla baada ya kuuawa kwa Kiongozi huyo wa ugaidi.

**WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

**304. MHESHIMIWA ASAA OTHMAN HAMAD (B.L.W):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- MKURABITA ni dhana mahsusi ya Serikali iliyokusudiwa kuondoa umasikini nchini hasa kwa Wananchi

wanaoishi vijijini; dhana hii ilijengwa kwa kauli nyingi zikiwemo “Kilimo ni uti wa mgongo”, “Kilimo ni Uhai” na “Kilimo kwanza”:-

(a) Je, Serikali ina kauli gani kwa wakulima waliozitumikia kauli mbiu hizo kwa kuzalisha mazao mengi ya kilimo na hatimaye kukosa masoko;

(b) Je, kwa nini Serikali isiwalipe fidia Wakulima walioathirika kiuchumi kwa kukosa masoko ya mazao waliyozalisha.

**WIZARA YA UJENZI:**

**305. MHESHIMIWA FAITH MOHAMED MITAMBO (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:- Mwaka 2010, Mhe Rais aliahidi kuwajengea Wananchi wa Liwale barabara ya kutoka Liwale hadi Kingupira kupitia *Selous Game Reserve*:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza.

## WIZARA YA MAJI:

**306. MHESHIMIWA DAVID ERNEST SILINDE (MBOZI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-
Wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa mwaka 2010; Mheshimiwa Rais aliahidi kuwapatia maji salama na ya uhakika Wananchi wa Tunduma lakini mpaka sasa muda wa Rais kutawala unamalizika na ahadi hiyo bado haijatekelezwa:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa kama Rais alivyoahidi.

**307. MHESHIMIWA AUGUSTINO MANYANDA MASELE (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-
Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Serikali kupitia Wizara ya Maji ilikuwa imetenga katika bajeti yake fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa ajili ya vijiji vya Ilolangulu, Iponya na Kijiji cha Lugunga:-

(a) Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha miradi hii ambayo ni muhimu sana;

(b) Kwa kuwa, Mradi wa Masumbwe Wilaya ya Mbogwe hautoi maji kwa muda mrefu; Je, ni lini Serikali itatoa kiasi cha shilingi milioni 200 ilizoahidi kwa ajili ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**308. MHESHIMIWA RACHEL ROBERT MASHISHANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Kumekuwepo na malalamiko makubwa juu ya unyanyasaji unaofanywa na mwekezaji wa shamba la Mkonge la Kumburu chini ya umiliki wa Kampuni ya SILVER GENERAL DISTRIBUTORS LTD dhidi ya wanavijiji wa Ngome na Kwamnyefu; Mwekezaji huyo amekaidi amri ya Naibu Waziri wa Ardhi wakati huo (2012) kuwa shamba la Kumburu lipimwe upya na kuweka mipaka na ramani kwa eneo linalodaiwa na wanakijiji ili wapewe ardhi yao:-

(a) Je, ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali dhidi ya Mwekezaji huyo;

(b) Je, ni lini ramani na mipaka ya shamba hilo itawekwa ili kumaliza ugomvi baina ya pande hizo.

**309. MHESHIMIWA ROSWEETER FAUSTIN KASIKILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

(a) Sheria ya Ardhi Namba 4 na Sheria ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999 zinazingatia haki za Wanawake katika umiliki wa mali na ushiriki wao katika Kamati za Ardhi:-

(b) Je, ni Wanawake wangapi wa vijiji gani katika Mkoa wa Rukwa wameelimishwa juu ya Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Vijiji Namba 5.

## WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

**310. MHESHIMIWA LOLESIA MASELLE BUKWIMBA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka huduma au utoaji dawa za UKIMWI katika Zahanati na Vituo vya Afya.

**311. MHESHIMIWA RIZIKI OMAR JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Taasisi ya Mifupa ya MOI ina deni la Tshs. Bilioni moja kwa MSD mpaka sasa inafikia kufungiwa kupata vifaa bila kutoa fedha:-

Je, ni lini Serikali italipa deni hilo ili vifaa viweze kupatikana bila masharti.

## II. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

**(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge zima na kusomwa Mara ya Tatu)**

Muswada wa Sheria ya Kuwalinda watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi wa Mwaka 2015 (*The Whistleblower and Witness Protection Bill, 2015)*

***(Majadiliano yanaendelea katika ngazi ya Kamati ya Bunge zima)***

Muswada wa Sheria ya Petroli wa Mwaka 2015(*The Petroleum Bill, 2015*).

Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi wa Mwaka 2015(*The Oil and Gas Revenue Management Bill, 2015*).

Muswada wa Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uchimbaji Tanzania wa Mwaka 2015 [*The Tanzania Extractive Industry (Transparency and Accountability) Bill, 2015*].

**DODOMA**
**03 JULAI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**